MPYAA.

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA AFYA

**MKOA WA KAGERA**
Anwani:"AFYA"
Simu Na: 028-2220927
Telefax Na: 028- 2221425
E.mail: bukobarrh@afya.go.tz

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Bukoba
S.L.P 265,
**BUKOBA.**

Unapojibutafadhalitaja:

Kumb. Na.AB.72/174/01C/91 10 Oktoba, 2023

Kuh: **TANGAZO LA NAFASI ZA AJIRAYA MKATABA**

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Bukoba, anawaalika Watanzania wenye sifa kuomba nafasi ya kazi ya mkataba katika nafasi zifuatazo:-

### 1. MHANDISI WA UJENZI (CIVIL ENGINEER) DARAJA II – NAFASI 1

**Sifa za mwombaji:**
Awe mwenye Shahada katika fani ya Uhandisi wa Ujenzi kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali, mwenye uzoefu walau mwaka mmoja.

**Kazi na Majukumu:**

Kutambua maeneo yanayoweza kufanyiwa Ukarabati pamoja na kutunza na kuhifadhi taarifa mbalimbali za majengo.

i) Kuandaa mipango kazi ya Kaguzi za Majengo mbalimbali.
ii) Kuandaa ripoti ya utafiti wa awali pamoja na Mipango ya Kazi itakayosaidia katika kufanya Ukaguzi wa Ufanisi wa majengo ya taasisi.
iii) Kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukarabati wa majengo ya Hospitali
iv) Kuandaa taarifa za ufuatiliaji wa mapendekezo ya ukarabati ndani ya Hospitali
v) Kutayarisha bajeti ya mwaka ya ujenzi na matengenezo ya miundombinu ndani ya hospitali.
vi) Kusimamia na kuratibu kazi za majengo ndani ya Hospitali
vii) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na msimamizi wake wa kazi.

Dkt. MN/ec*

CamScanner

MPYAA

## 2. DAKTARI DARAJA LA II – NAFASI 2

**Sifa za mwombaji:**
Awe na leseni/amesajiliwa na Baraza la Madaktari Tanzania.

**Kazi na Majukumu:**

i) Kufanya kazi zote za matibabu hospitalini zinazohusiana na magonjwa mbalimbali yakiwemo magonjwa ya watoto, magonjwa akina mama na upasuaji wa kawaida na wa dharura.
ii) Kutoa na kusimamia elimu ya afya pamoja na kuboresha afya ya jamii katika Wialaya na Mikoa au eneo lake la kazi.
iii) Kuchunguza, kufuatilia na kuzuia milipuko ya magonjwa.
iv) Kutunza takwimu na kuzitumia kama inavyoelekezwa katika misingi ya MUTHA.
v) Kupanga na kutathimini huduma za afya katika eneo lake la kazi.
vi) Kufundisha wanafunzi na watumishi waliopo kwenye eeo la kazi
vii) Kusimamia na kuelekeza wafanyakazi walio chini yake
viii) Kufundisha wanafunzi katika vyuo vya afya vilivyopo eneo lake la kazi.
ix) Kubuni na kuendesha utafiti na kusambaza matokeo
x) Kubuni na kutayarisha mikatakati ya kuinua ubora wa huduma ya fani yake.
xi) Kuandaa mipango na makisio ya bajeti ya huduma za afya
xii) Kushiriki, kuhakiki na kuboresha huduma za afya (medical audit and quality improvement).
xiii) Kutoa huduma za outreach katika wilaya/Mkoa wake.
xiv) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

## 3. MUUGUZI II - NAFASI 2

**Sifa za mwombaji:**

- Awe na elimu ya kidato cha nne na Astashahada ya Uuguzi kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali.
- Awe ameandikishwa (Enrolled) na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania

**KAZI NA MAJUKUMU**

i) Kufanya kazi za kiuguzi za kuhudumia wateja katika jamii, hospitali na
ii) sehemu zote zinapotolewa huduma za afya.
iii) Kusimamia na kuratibu kazi zote za wahudumu wa afya katika sehemu yake ya kazi
iv) Kukusanya takwimu na kutayarisha taarifa za utendaji wake wa kazi
v) Kutoa huduma kwa wagonjwa majumbani
vi) Kutoa ushauri nasaha
vii) Kutoa huduma za kinga na uzazi wa mpango
viii) Kutoa huduma za uzazi ya mama na mtoto
ix) Kuelimisha wagonjwa na jamii kuhusu matatizo yao ya kiafya
x) Kufuatilia utunzaji wa vitendea kazi katika maeneo yake ya kazi
xi) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.



CamScanner

MPYAA

## 4. DEREVA II NAFASI 1

**Sifa za mwombaji:**

Awe mwenye elimu ya kidato cha nne na Astashahada katika fani yake kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali.

**KAZI NA MAJUKUMU:**

i) Kuhakikisha anatunza gari kwa usafi na salama wakati wote
ii) Kuwaendesha viongozi
iii) Kutoa taarifa ya matatizo/matengenezo ambayo yatakuwa yanahitajika
iv) Kutunza nyaraka zote muhimu za gari
v) Kuhakikisha matengenezo ya gari yanafanyika kwa wakati
vi) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi.

**MASHARTI YA KAZI;**

I. Ajira itakuwa ni ya mkataba wa mwaka mmoja.
II. Baada ya kipindi cha mkataba kuisha, Mfanyakazi atakayekuwa ameonesha ufanisi katika utendaji mkataba wake utaweza kuhuishwa.

**Mambo ya kuzingatia kwa waombaji**

I. Ni Mtanzania
II. Hajawahi kufungwa kwa makosa ya jinai
III. Hajawahi kufukuzwa/kupunguzwa toka Serikalini
IV. Umri kuanzia miaka 21 hadi 45.

**Barua zote za maombi ziambatishwe na vivuli vya vyeti vya kuzaliwa, kitambulisho cha uraia, vyeti vya elimu na ujuzi, Maelezo binafsi (CV) yaliyoambatana na wadhamini wawili pamoja na picha moja (1) ya rangi (Passport size).**

**MAOMBI YOTE YATUMWE KWA**
Mganga Mfawidhi,
Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Bukoba,
S.L.P 265,
**BUKOBA.**

**MWISHO WA KUTUMA MAOMBI NI TAREHE: 24/10/2023 SAA 9:00 ALASIRI.**

Dkt. Museleta Nyakiroto
**MGANGA MFAWIDHI**
**HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA, BUKOBA**

Dkt.MN/ec*

CamScanner